

East African Currency...

This will definitely take you back to some old memories!

Hope that you haven't forgotten your Swahili...

**From German to Gt. Britain gov'ts, check out the old E.
A. currency -**

from 1900s to late 1900s.

Some of the info. is in Kiswahili. Happy nostalgia!



Rupie 10



Rupie 50





Rupie 100



Kwa upande wa zanzibar, mwaka huo huo wa 1905, noti za Rupee za kizanzibari zilitolewa katika thamani za Rupee 5, 10, 20, 50, 100 na rupee 500 pia. Kwa bahati mbaya sikuweza kupata picha zake zote, naonyesha mfano wa noti za rupee 5 tano tu niliyofanikiwa kupata.

5 Zanzibari rupee



Wakati wa vita ya kwanza ya dunia, serikali ya kijerumani ilitoa noti za dharura ambazo zilikuwa ni za karatasi ya kawaida kabisa. Noti hizi zilikuwa katika thamani za Rupie 1, 5, 10, 20, 50 and Rupie 200 ingawa hizi za Rupie 200 zilikuwa adimu sana na sikufanikiwa kupata picha yake

1 Rupie



5 Rupien




10 Rupien





20 Rupien



50 Rupien



Noti hizi za dharura zili kuwa hafifu sana na wakati mwingine zili kuwa zinayatuliwa kwa muhuri tu kama hii hapa chini ya Rupie 1.



Inaelekea kuwa mji wa Tabora ulikuwa na umuhimu wa pili kwa dar es salaama wakati wa serikali ya kijerumani kwa vile unaonyeshwa katika Noti zote. Kama mtakumbuka, ile sarafu ya dhahabu ya Rupie 15 ilikuwa inaitwa "Tabora Pound."

.....INAENDELEA

Last edited by Kichuguu; 4th September 2007 at 02:32 AM..

Views: 1934

[Quote](#)

The Following 11 Users Say Thank You to Kichuguu For This Useful Post:

Wakati wa Utawala wa Mwingereza

Baada ya utawala wa kijerumani kuanguka na nchi kuchukuliwa na waingereza, kwanza nchi ilitumia noti za Rupee za Afrika ya Mashariki na Rupee za Zanzibar ingawa Rupie za kijerumani pia ziliendelea kutumika. Kwa upande wa Zanzibar noti ya rupee 1 ilianzishwa mwaka 1920. baadhi ya noti hizo ni hizi hapa


1 Zanzibari Rupee




1 EA Rupee



5 EA Rupee



10 EA Rupee



Katikati ya mwaka 1920, serikali ya uingereza ilianzishwa sarafu ya pamoja kwa nchi zote za Afrika ya Mashariki iliojuliakana kama Florin ya Afrika ya Mashariki. Noti za Florini zilikuwa katika thamani za Florin 1, 5, 10, 20, 50, 100 na Florin 500, ambapo noti za kuanzia Florin 10 na kuendelea juu zilikuwa pia na thamani ya Pound (1, 2, 5, 10 na 50). Kwa vile sarafu hii haikudumu zaidi ya miezi sita, ni noti chache sana zilizotolewa, mifano ya noti hizo ni kama ifuatavyo

1 EA Florin



5 EA Florin



Mwanzoni mwa mwak 1921, serikali ya kiingereza ilianzisha sarafu ya pamoja afrika mashariki iliyojulikana kama Shillingi ya Afrika ya Mashariki na hivyo kuondokana na Florin ya Afrika Mashariki. Shilingi ya Afrika Mashariki (baadaye nitakuwa naandika kwa kifupi tu kama Shilling) ilikuwa na thamani ya Shillingi 20 kwa pound moja na ilikuwa imeegesha kwenye pound kiasi kuwa thamani ya Shilling 20 kwa pound haikubadilika. Noti za Shillingi zilizotolewa wakati huo zilikuwa za thamani za Shillingi 5, 10, 20, 100, 1000, na Shillingi 10,000. Noti za Shillingi ishirini na kuendelea juu zilikuwa pia na thamani ya pound (1, 5, 50). Noti hizi zilikuwa zimeandikwa kwa kiingereza, kiarabu na kiamhara kinachotumika Ethiopia. Katika utawala wote wa kiingereza, kulitolewa mitindo miwili tu ya noti hizo. Mtindo wa kwanza ulidumu kuanzia mwaka 1921 hadi mwaka 1958, ma mtindo wa pili ulidumu kuanzia mwaka 1958 hadi baada ya uhuru mwaka 1964. Sura ya mbele ya noti zote ilikuwa ikionyesha mtawala wa himaya ya uingereza. Sura ya nyuma kwa upande wa noti za mtindo wa kwanza ilikuwa na simba mmoja wa kiume katika eneo la mlima Kenya. Noti zilizotolewa mara ya kwanza wakati wa utawala wa Mfalme George wa tano (1910-1936) ni kama ifuatavyo:

5 EA Shilling



10 EA Shilling



20 EA Shilling



100 EA Shilling



1000 EA Shilling




(Picha hii ilipingwa wakati pesa imeshafutwa rasmi kwa kutobolewa matundu; noti halisi haikuwa na matundu hayo)

Kwa thamani ya shillingi na uchumi wa watu wakati huo, ni noti chache sana zenyé thamani ya Shilling 1000 na Shillingi 10,000 ziliingia kwenye mzunguko, na sikufanikiwa kupata noti ya Shilingi 10,000. Kwa hiyo ilipofika mwaka 1933, serikali ikaamua kusimaisha matumiz ya noti za shillingi 1000 ingawa zile za shillingi 10,00 ziliendelea. Wakati wa utawala mfupi wa Mfalme Edward wa nane mwaka 1936, hazikutolewa noti zozote. Noti nyingine zilitolewa wakati wa utawala wa mfame George wa sita (1936-1952), ambapo noti ya Shillingi 1 ilianzishwa. Noti hizo zilikuwa kama ifuatavyo.

1 EA Shilling




5 EA Shilling



10 EA Shilling



20 EA Shilling



100 EA Shilling




Kutokana na uhadimu wake, sikuweza kupata noti za Shillingi 10,000. Hata hivyo miaka 11 ndani ya utawala wa mfalme George wa sita, iliamuliwa kufuta noti hizi za Shillingi 10,000 ambazo zilikuwa hazitumiki sana.

Baada ya kifo cha Mfalme George wa sita mwaka 1952 na binti yake Malkia Elizabeth wa pili kuchukua usukani noti zilizotolewa zilikuwa zinafanana na zile zilizokuwapo mwazoni isipokuwa aliondoa noti ya Shillingi 1 kwenye mzunguko.



5 EA Shilling




10 EA Shilling



20 EA Shilling



100 EA Shilling




.... INAENDELEA

#3 ([permalink](#))

Hata hivyo mwaka 1958, noti hizo zilitengezwa upya katika mtindo tofauti na zile zilizokuwapo mwanzo. Noti mpya ziliwa na rangi nyinyi huku zikonyesha mazao mbali mbali ya uchumi yaliyokuwapo Afrika ya Mashariki. Noti ya shillingi 5 ilionyesha pamba na karafuu; noti ya shillingi 10 ilionyesha mkonge na chai; noti ya shillingi 20 ilionyesha kahawa na alizeti, na mwisho noti ya shillingi 100 ilionyesha minazi, miwese na pareto. Inaelekea kuwa kuanzia hapo, shillingi ya Afrika mashariki iliachaa kubebeshwa kwenye pound kwa vile noti mpya hazikuwa na thamani ya pound tena.


5 EA Shilling



10 EA Shilling



20 EA Shilling



100 EA Shilling




Noti hizi ziliendelea hadi baada ya uhuru ingawa mwaka 1961 zilifanyiwa marekebsihao madogo kwenye sura ya mbele ili kuweza kuonyesha sahihi sita za wajumbe wa bodi ya fedha ya afrika mashariki ambapo wakati huo walikuwa wameongezeka na kuwa sita kutoka watano waliokuwapo mwaka 1958. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo

5 EA Shilling



10 EA Shilling



20 EA Shilling




100 EA Shilling



Baada ya nchi zote za Afrika ya Mashariki kuwa huru, noti za kwanza zilizotolewa mwaka 1964 zilifanyiwa mabadiliko makubwa sana. Kwanza, noti hizi zilikuwa zimeandikwa katika kiingereza, kiarabu na kishwahili; halafu sura ya mtawala wa uingereza iliondolewa na badala yake kuwekwa mashua. Sikuweza kufahamu mara moja kwa nini waliamua kutumia mashua. Sura za nyuma za noti ziliendelea kuonyesha mazao mbalimbali ya Afrika ya Mashariki ingawa kwa mpangilio tofauti kama inonekanavyo katika picha hizi.

5 EA Shilling



10 EA Shilling



20 EA Shilling



100 EA Shilling



..... INAENDELEA